# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza Kutumika.
2. Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA AJIRA, NAM. 11 YA MWAKA 2005**

3. Kusomwa.
4. Marekebisho ya kifungu cha 36.
5. Marekebisho ya kifungu cha 37.
6. Kuongezwa kifungu kipya cha 44A.
7. Kuongezwa kifungu kipya cha 123A.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI, NAM. 8 MWAKA 2015**

8. Kusomwa.
9. Marekebisho ya kifungu cha 9.
10. Marekebisho ya kifungu cha 14.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA YA KARUME, NAM. 2 YA MWAKA 2009**

11. Kusomwa.
12. Marekebisho ya kifungu cha 2.

13. Marekebisho ya kifungu cha 3.

14. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 4.

15. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 5.

16. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 6

17. Marekebisho ya kifungu cha 7.

18. Marekebisho ya kifungu cha 8.

19. Marekebisho ya kifungu cha 10.

20. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 11.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAFIRI BARABARANI, NAM. 7 YA MWAKA 2003

21. Kusomwa.

22. Marekebisho ya kifungu cha 16G.

23. Marekebisho ya kifungu cha 43.

24. Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 202A.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI, NAM. 12 YA MWAKA 1992

25. Kusomwa.

26. Marekebisho ya kifungu cha 2.

27. Marekebisho ya kifungu cha 3.

28. Marekebisho ya kifungu cha 33.

29. Marekebisho ya kifungu cha 47.

30. Kuongezwa kifungu kipya cha 65A.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KAMISHENI YA ARDHI, NAM. 6 YA MWAKA 2015


31. Kusomwa.

32. Marekebisho ya kifungu cha 6.

33. Marekebisho ya kifungu cha 4.

34. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 28.

35. Kufuta kifungu cha 29.


## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR NAM. 6 YA MWAKA 2012


36. Kusomwa.

37. Marekebisho ya kifungu cha 3.

38. Marekebisho ya kifungu cha 4.

39. Marekebisho ya kifungu cha 5.

40. Marekebisho ya kifungu cha 6.

41. Marekebisho ya kifungu cha 8.

42. Kuongezwa vifungu vipya vya 22A na 22B.


## SEHEMU YA TISA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU, NAM. 10 YA MWAKA 2018


43. Kusomwa.

44. Marekebisho ya kifungu cha 8.

45. Marekebisho ya kifungu cha 10.

46. Marekebisho ya kifungu cha 12.

47. Marekebisho ya kifungu cha 19.

48. Marekebisho ya kifungu cha 20.

49. Marekebisho ya kifungu cha 22.

50. Marekebisho ya kifungu cha 32.

51. Marekebisho ya Jadweli.


## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

52. Kusomwa.

53. Marekebisho ya kifungu cha 26.

54. Marekebisho ya kifungu cha 29.

55. Marekebisho ya kifungu cha 31.

56. Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.


## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA VYOMBO VYA MOTO VYA SERIKALI, NAM. 13 YA MWAKA 2004

57. Kusomwa.

58. Marekebisho ya kifungu cha 2.

59. Marekebsiho ya kifungu cha 3.

60. Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.


## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUMO WA UDHIBITI WA LESENI ZA BIASHARA, NAM. 13 YA 2013

61. Kusomwa.

62. Marekebisho ya kifungu cha 5.

63 Marekebisho ya kifungu cha 51.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA, NAM. 3 YA 2016


64. Kusomwa.

65. Marekebisho ya kifungu cha 5.

66. Kuongeza kifungu kipya cha 5A.

**SHERIA NAM. 5 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

21 Julai, **2022**

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza Kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2022 na itaanza kutumika mara baada ya kuwekwa saini na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA AJIRA, NAM. 11 YA MWAKA 2005

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ajira, Nam. 11 ya Mwaka 2005 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 36.

**4.** Kifungu cha 36 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa kifungu kidogo cha (6) na kuwekwa badala yake kifungu kidogo kipya cha (6) kama ifuatavyo:

"(6) Kwa madhumuni ya ajira chini ya Sheria hii, mgeni yeyote atakayefunga ndoa na Mzanzibari kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazokubalika Zanzibar na ambaye kwa kawaida ni mkaazi wa Zanzibar kwa angalau miaka mitatu hatachukuliwa kama ni mgeni iwapo ana barua ya utambulisho iliyotolewa na Kamishna";

(b) kuongezwa kifungu kidogo kipya cha (7) mara baada ya kifungu kidogo cha (6) kama ifuatavyo:

"(7) Barua maalum ya utambulisho iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki, itakuwa halali kwa kipindi cha kibali cha kazi na inaweza kufanywa tena kwa kipindi chengine baada ya kufanya maombi kwa Kamishna";

(c) kukipa nambari mpya kifungu kidogo cha (7) kuwa kifungu kidogo cha (8).

Marekebisho ya kifungu cha 37.

**5.** Kifungu cha 37 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kufutwa maneno "miezi sita hadi kumi na mbili" na kuwekwa badala yake maneno "miezi sita hadi miaka miwili";

(b) katika kifungu kidogo cha (2) kinarekebihwa kwa:

(i) kufutwa maneno "si zaidi ya mwaka mmoja kwa wakati" na kuweka badala yake maneno "kipindi chengine".

(ii) kufutwa maneno "Sheria ya Kukuza na kulinda Uwekezaji Zanzibar, 2004" na kuwekwa badala yake maneno "Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar".

Kuongezwa kifungu kipya cha 44A.

**6.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 44A mara baada ya kifungu cha 44 kama ifuatavyo:

"Kuchukuwa wanafunzi wa vitendo.

**44A.** Bila ya kuathiri masharti ya sheria nyengine yoyote, mwajiri yeyote atakayechukuwa mwanafunzi wa vitendo katika taasisi yake atafuata utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Kuongezwa kifungu kipya cha 123A.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 123A mara baada ya kifungu cha 123 kama ifuatavyo:

"Kumaliza kosa.

**123A.**-(1) Kamishna anaweza kumaliza kosa lililofanywa na mtu chini ya Sheria hii au Kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, iwapo, mtu huyo:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa na atachukuwa tahadhari kwa kutorudia tena kosa; na

(b) atalipa malipo yote chini ya Sheria hii.

(2) Ikiwa kesi ya jinai imefunguliwa dhidi ya mtu, mamlaka yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayatatumika bila ya kupata ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar.

(3) Utozaji wa faini chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hautachukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na iwapo malipo ya msingi yamelipwa yote, hakutakuwa na mashtaka kwa kosa linaloshukiwa ambalo litafunguliwa au kuendelezwa".

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI, NAM. 8 MWAKA 2015

Kusomwa.

**8.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Nam. 8 ya Mwaka 2015 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**9.** Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufutwa maneno "Tume ya Mipango Zanzibar" na kuwekwa badala yake maneno "Wizara inayohusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

Marekebisho ya kifungu cha 14.

**10.** Kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufutwa aya ya (b) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (b) kama ifuatavyo:

"(b) mwakilishi atakayeteuliwa kutoka Wizara inayohusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA YA KARUME, NAM. 2 YA MWAKA 2009

Kusomwa.

**11.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Nam. 2 ya Mwaka 2009 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**12.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa tafsiri ya neno "Mrajis".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**13.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa maneno "na vitu" katika aya ya (f) ya kifungu kidogo cha (2);

(b) kufutwa vifungu vidogo vya (3) na (4).

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 4.

**14.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 4 kama ifuatavyo:

"Idara za Taasisi.

**4.**-(1) Taasisi itajumuisha Idara kama Baraza litakavyoamua.

(2) Baraza linaweza kuteua Wakuu wa Idara za Taasisi baada ya kupata mapendekezo ya Mkuu wa Taasisi.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya pili katika fani ya sayansi na teknolojia kutoka katika taasisi inayotambuliwa; na

(b) ana angalau uzoefu wa kazi wa miaka mitatu katika taasisi ya kitaaluma.

(4) Wakuu wa Idara watashikilia nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(5) Kazi za Wakuu wa Idara zitakuwa:

(a) kumsaidia na kumshauri Mkuu na Naibu Wakuu wa Taasisi katika kushughulikia shughuli za Kitaaluma na zisizo za Kitaaluma;

(b) kuratibu na kudhibiti shughuli zote za mitihani za idara;

(c) kusimamia miradi ya wanafunzi; na

(d) kusimamia masuala yote yanayohusiana na idara.

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 5.

**15.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 5 kama ifuatavyo:

"Kazi za Taasisi.

**5.** Kazi za Taasisi zitakuwa:

(a) kuhifadhi, kuimarisha, kupeleka na kusambaza elimu ya sayansi na teknolojia kwa kufundisha, kufanya utafiti, uvumbuzi na ushauri katika maeneo mbali mbali;

(b) kuendeleza, kudumisha na kukuza sayansi na teknolojia katika viwango vya juu viwezekanavyo;

(c) kutoa nyenzo kwa ajili ya kufundishia, kuongeza muda na mafunzo katika maeneo ya teknolojia na masuala mengine yote ya sayansi kwa mujibu wa kanuni za kisayansi za kisasa;

(d) kuwasiliana na kushirikiana na vyuo vyengine vya elimu ya juu katika kuendeleza na kuleta maendeleo ya sayansi na teknolojia;

(e) kuandaa na kuratibu ufundishaji wa sayansi na teknolojia katika ngazi mbali mbali ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa ndani na nje wanaojiunga na Taasisi;

(f) kukuza kipato;

(g) kufanya mitihani kwa ajili ya kutoa Shahada, Stashahada, Cheti na tuzo nyengine za Taasisi kama ilivyoidhinishwa na Bodi ya Taaluma;

(h) kutoa huduma za ushauri kwa sekta ya umma na binafsi katika maeneo maalum kama ilivyoainishwa katika Sheria hii;

(i) kufadhili, kupanga, kuwezesha na kutoa vifaa kwa ajili ya mikutano, makongamano, mikutano, semina na warsha kwa ajili ya majadiliano ya mambo yanayohusiana na maendeleo ya sayansi na teknolojia;

(j) kutoa Cheti, Stashahada, Shahada na tuzo nyengine wenyewe au kama mshirika au wakala wa taasisi nyengine yoyote ama ya ndani au nje ya nchi kama itakavyoidhinishwa na Baraza;

(k) kushirikiana na chuo au taasisi inayotoa kozi za sayansi na teknolojia ama ndani au nje ya Zanzibar;

(l) kuendeleza Watumishi wa Taasisi kitaaluma; na

(m) kufanya jambo lolote ambalo ni la lazima au linalofaa au linaloambatana na madhumuni ya kazi zake".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 6.

**16.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 6 kama ifuatavyo:

"Kuanzishwa kwa Baraza.

**6.**-(1) Kutakuwa na Baraza la Taasisi ambalo litajumuisha:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkuu wa Taasisi ambaye atakuwa mjumbe kwa nafasi yake;

(c) Wajumbe wanane ambao watateuliwa na Waziri kwa kuzingatia uzoefu na elimu baada ya kushauriana na taasisi zinazohusika kama ifuatavyo:

(i) Mjumbe kutoka Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar;

(ii) Mjumbe kutoka taasisi yoyote ya elimu ya juu mwenye uzoefu katika Sayansi na Teknolojia au Uhandisi Zanzibar;

(iii) Mjumbe kutoka Wizara yenye dhamana ya elimu;

(iv) Mjumbe kutoka jumuiya ya wafanyabiashara;

(v) Mjumbe kutoka jumuiya ya wafanyakazi;

(vi) Mjumbe ambae ni mwakilishi kutoka Jumuiya ya Wanafunzi ya Taasisi;

(vii) Mjumbe ambae ni mwakilishi kutoka wafanyakazi wa kitaaluma wa Taasisi; na

(viii) Mjumbe mwengine mmoja mwenye uzoefu katika elimu.

(2) Wajumbe wa Baraza watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza.

(3) Baraza litamteua Afisa wa Umma ambaye atakuwa na sifa zifuatazo kuwa Katibu wa Baraza:

(a) awe ana angalau Shahada ya Kwanza kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) awe muadilifu wa hali ya juu;

(a) awe na uwezo wa kutumia vifaa vya Teknologia na Habari; na

(d) awe anaweza kutunza siri.

(4) Katibu atakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuchukuwa kumbukumbu sahihi za mikutano ya Baraza;

(b) kutunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Baraza;

(c) kutoa taarifa sahihi za mikutano ya Baraza kwa wajumbe;

(d) kutoa ushauri sahihi kwa Baraza pale unapohitajika; na

(e) kufanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Baraza".

(5) Isipokuwa Wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na Wajumbe wengine wa Baraza watashika nafasi kwa

kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu".

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**17.** Kifungu cha 7 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufutwa aya ya (h) na kuwekwa aya mpya za (h) na (i) kama ifuatavyo:

"(h) kuteua Wakuu wa Idara baada ya kupata mapendekezo ya Mkuu wa Taasisi;

(i) kufanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Waziri".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**18.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (1) na kuwekwa badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Baraza litaanzisha Bodi ya Taaluma ambayo itajumuisha:

(a) Mkuu wa Taasisi ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Naibu Mkuu wa Taasisi wa Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri wa Taasisi ambaye atakuwa Katibu;

(c) Naibu Mkuu wa Taasisi wa Utawala, Mipango na Fedha wa Taasisi;

(d) Wakuu wote wa Idara za Kitaaluma za Taasisi;

(e) Afisa Uhusiano wa Viwanda wa Taasisi;

(f) Mkuu wa Wanafunzi;

(g) Afisa Sheria wa Taasisi; na

(h) Mwakilishi wa Jumuiya ya Wanafunzi.

Marekebisho ya kifungu cha 10.

**19.** Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa neno "Mkurugenzi" liliopo katika kifungu kidogo cha (1) na badala yake kuwekwa neno "Mkuu wa Taasisi" na marekebisho haya yatafanyika popote ambapo neno "Mkurugenzi" limejitokeza katika Sheria Mama.

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 11.

**20.** Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 11 kama ifuatavyo:

"Kuteuliwa kwa Naibu Wakuu.

**11.-**(1) Kutakuwa na Naibu Mkuu wa Taasisi wa Utawala, Mipango na Fedha na Naibu Mkuu wa Taasisi wa Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri wa Taasisi ambao watateuliwa na Rais.

(2) Naibu Mkuu wa Taasisi wa Utawala, Mipango na Fedha na Naibu Mkuu wa Taasisi wa Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri watateuliwa kwa njia ya ushindani wa kuajiri kwa mujibu wa masharti kama Rais atakavyoamua.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Taasisi wa Utawala, Mipango na Fedha ikiwa mtu huyo ana:

(a) Shahada ya Tatu katika fani ya utawala, uchumi, sheria na fani yoyote inayolingana na hizo kutoka katika taasisi inayotambulika; na

(b) uzoefu wa kiutawala kwa angalau miaka mitatu katika taasisi ya kitaaluma.

(4) Naibu Mkuu wa Taasisi wa Utawala, Mipango na Fedha:

(a) atakuwa Msaidizi Mkuu na Mshauri Mkuu wa Mkuu wa Taasisi katika mambo yote yanayohusiana na utawala, mipango na fedha za Taasisi;

(b) atatekeleza majukumu mengine kama alivyokabidhiwa na Mkuu wa Taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(c) atasimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi pamoja na miongozo inayotolewa na Taasisi;

(d) atasimamia Idara iliyopo chini yake; na

(e) atasimamia mambo yote yanayohusiana na utawala kama itakavyoagizwa na Mkuu wa Taasisi au Baraza".

(5) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Taasisi wa Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri ikiwa mtu huyo ana:

(a) Shahada ya Tatu katika fani ya sayansi na teknolojia au uhandisi kutoka katika taasisi inayotambulika; na

(b) uzoefu wa kiutawala kwa angalau miaka mitatu katika taasisi ya kitaaluma.

(6) Naibu Mkuu wa Taasisi wa Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri:

(a) atamshauri Mkuu wa Taasisi juu ya taaluma na mambo ya kitaaluma;

(b) atawasilisha matokeo ya mitihani kwenye Bodi ya Taaluma na kuyawasilisha katika Baraza la Taasisi;

(c) atasimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi pamoja na miongozo inayotolewa na Taasisi;

(d) atasimamia Idara iliyopo chini yake;

(e) atakuwa kiungo miongoni mwa idara; na

(f) atawasilisha ripoti ya matokeo ya kila muhula katika Mamlaka husika.

(7) Naibu Mkuu wa Taasisi wa Utawala, Mipango na Fedha na Naibu Mkuu wa Taasisi wa Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa kwa kipindi chengine.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAFIRI BARABARANI, NAM. 7 YA MWAKA 2003

Kusomwa.

**21.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usafiri Barabarani, Nam. 7 ya Mwaka 2003 ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu 16G.

**22.** Kifungu cha 16G cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (1) na kuwekwa badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Kunaanzishwa Kamati ya Usalama Barabarani ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Mkuu kutoka Wizara inayohusika na usafiri wa barabarani ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Katibu Tawala wa kila Mkoa wa Zanzibar;

(c) Mjumbe kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mwenye cheo cha Mkurugenzi ambaye atateuliwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo;

(d) Mkurugenzi anayehusika na Mipango, kutoka Wizara inayohusika na usafiri wa barabarani;

(e) Mjumbe kutoka Wizara inayohusika na elimu mwenye cheo cha Mkurugenzi ambaye atateuliwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo;

(f) Mjumbe kutoka Wizara inayohusika na afya mwenye cheo cha Mkurugenzi ambaye atateuliwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo;

(g) Mkuu wa Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani Zanzibar;

(h) Mwenyekiti wa Kitaifa wa Jumuiya ya Usafiri wa Barabara Zanzibar; na

(i) Mkurugenzi Mkuu".

Marekebisho ya kifungu cha 43.

**23.** Kifungu cha 43 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (2), kufutwa aya ya (b) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (b) kama ifuatavyo:

"(b) haitotolewa kwa gari za usafiri wa umma";

(b) kuongezwa kifungu kidogo kipya cha (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, gari au trela iliyosajiliwa Tanzania Bara inaweza kutumika Zanzibar kwa utaratibu utakaowekwa katika kanuni".

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 202A.

**24.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 202A mara baada ya kifungu cha 202 kama ifuatavyo:

"Uwezo wa kumaliza kosa.

**202A.-**(1) Mamlaka inaweza kumaliza kosa lililofanywa na mtu chini ya Sheria hii au Kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, iwapo, mtu huyo:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa na atachukuwa tahadhari kwa kutorudia tena kosa; na

(b) atalipa malipo yote chini ya Sheria hii.

(2) Ikiwa kesi ya jinai imefunguliwa dhidi ya mtu, uwezo uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hautatumika bila ya kupata ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar.

(3) Utozaji wa faini chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hautachukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na iwapo kwamba malipo ya msingi yamelipwa yote, hakutakuwa na mashtaka kwa kosa linaloshukiwa ambalo litafunguliwa au kuendelezwa".

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI, NAM. 12 YA MWAKA 1992

Kusomwa.

**25.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Umiliki wa Ardhi, Nam. 12 ya Mwaka 1992 ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**26.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongezwa ufafanuzi wa neno "Kamisheni" katika mpangilio wa kiherufi kama ifuatavyo:

"Kamisheni" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Kamisheni ya Ardhi, Nam. 6 ya Mwaka 2015.

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**27.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (6).

Marekebisho ya kifungu cha 33.

**28.** Kifungu cha 33 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kufutwa maneno "hakutakuwa na haki ya kisheria" na kuwekwa badala yake maneno "hakuna uhaulishaji wa ardhi utakaoruhusiwa";

(b) kufutwa kifungu kidogo cha (2);

(c) kuzipa nambari upya aya zilizobakia kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 47.

**29.** Kifungu cha 47 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufutwa maneno "Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi" na kuwekwa badala yake maneno "Kamisheni".

Kuongezwa kifungu kipya cha 65A.

**30.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 65A mara baada ya kifungu cha 65 kama ifuatavyo:

"Idhini ya Rais katika ufutaji.

**65A.** Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, Waziri hatafuta haki yoyote ya matumizi ya ardhi au ukodishwaji wa ardhi bila ya kupata idhini ya Rais".

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KAMISHENI YA ARDHI, NAM. 6 YA MWAKA 2015

Kusomwa.

**31.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kamisheni ya Ardhi, Nam. 6 ya Mwaka 2015 ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**32.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa:

(a) kuongezwa aya mpya ya (d) mara baada ya aya ya (c) kama ifuatavyo:

"(d) kudhibiti uhaulishaji wa haki au maslahi ya ardhi iliyokuwa haijasajiliwa";

(c) kuzipa nambari upya aya zilizobakia kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**33.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa:

(a) kuongezwa aya mpya ya (d) mara baada ya aya ya (c) kama ifuatavyo:

"(d) Idara ya Mipango na Rasilimali Watu; na"

(b) kuipa nambari upya aya ya (d) kuwa aya ya (e).

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 28.

**34.** Kifungu cha 28 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 28 kama ifuatavyo:

"Kufuta na kubakiza.

**28.**-(1) Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi Nam. 8 ya 1994 inafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii".

Kufuta kifungu cha 29.

**35.** Kifungu cha 29 cha Sheria Mama kinafutwa.

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR NAM. 6 YA MWAKA 2012

Kusomwa.

**36.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Baraza la Mitihani la Zanzibar Nam. 6 ya Mwaka 2012 ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**37.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa maneno "Upimaji wa Elimu na Tathmini" na kuweka badala yake neno "Mitihani" katika kifungu kidogo cha (1);

(b) kufutwa neno "Baraza" katika aya za (a) na (d) na kuwekwa badala yake neno "Chombo" katika kifungu kidogo cha (2).

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**38.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa neno "skuli" na kuwekwa badala yake neno "elimu" katika aya ya (e) katika kifungu kidogo cha (1),

(b) kuongezwa maneno "kulingana na uzoefu na taaluma" mwishoni mwa kifungu kidogo cha (2).

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**39.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa aya za (a) na (b);

(b) kufutwa aya ya (k) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (k) kama ifuatavyo:

"(k) kufanya tathmini ili kujua ubora na mapungufu ya program za kielimu ili kuinua kiwango cha kujifunza kwa wanafunzi".

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**40.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongezwa aya mpya ya (m) mara baada ya aya (l) kama ifuatavyo:

"(m) kushirikiana na taasisi yoyote ya umma au ya binafsi kwa ajili ya utekelezaji mzuri kwa kazi zake alizopewa katika Sheria hii".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**41.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (1) na kuwekwa badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Isipokuwa kwa Wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na Wajumbe wengine wa Baraza watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu".

Kuongezwa vifungu vipya vya 22A na 22B.

**42.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa vifungu vipya vya 22A na 22B mara baada ya kifungu cha 22 kama ifuatavyo:

"Ulinzi na usalama wa mitihani.

**22A.**-(1) Baraza litashirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa katika kuhakikisha usalama wa mitihani.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, taratibu za ulinzi na usalama wa mitihani zitaainishwa katika Kanuni.

Mashirikiano na Kamati za Mitihani za Mikoa na Wilaya.

**22B.**-(1) Kutakuwa na Kamati za Mitihani za Mikoa na Wilaya kwa kila Mkoa na Wilaya za Zanzibar.

(2) Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitasimamia uendeshaji wa mitihani katika Mikoa na Wilaya husika.

(3) Kamati ya Mitihani ya Mkoa itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Tawala wa Mkoa ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati katika Mkoa husika;

(b) Afisa wa Elimu Mkoa ambaye atakuwa Katibu wa Kamati katika Mkoa husika;

(c) Afisa Sheria wa Mkoa;

(d) Kamanda wa Polisi wa Mkoa;

(e) Afisa Usalama wa Mkoa;

(f) Afisa wa Taaluma wa Mkoa; na

(g) Mwakilishi kutoka Idara Maalum.

(4) Kamati ya Mitihani ya Wilaya itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati katika Wilaya husika;

(b) Afisa wa Elimu Wilaya ambaye atakuwa Katibu wa Kamati katika Wilaya husika;

(c) Afisa Sheria wa Wilaya;

(d) Kamanda wa Polisi wa Wilaya;

(e) Afisa Usalama wa Wilaya;

(f) Afisa wa Taaluma wa Wilaya Msingi au Sekondari; na

(g) Mwakilishi kutoka Idara Maalum".

## SEHEMU YA TISA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU, NAM. 10 YA MWAKA 2018

Kusomwa.

**43.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Nam. 10 ya Mwaka 2018 ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**44.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Ripoti za ukaguzi zitawasilishwa kwa uongozi wa skuli na mamlaka husika kulingana na aina ya ukaguzi utakaofanyika ndani ya muda utakaoainishwa katika Kanuni za Ukaguzi".

Marekebisho ya kifungu cha 10.

**45.** Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufutwa aya ya (d) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (d) kama ifuatavyo:

"(d) Mwakilishi mwenye utaalamu na uzoefu katika masuala ya elimu miongoni mwa Walimu Wakuu kutoka katika skuli za Serikali".

Marekebisho ya kifungu cha 12.

**46.** Kifungu cha 12 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa aya (d) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (d) kama ifuatavyo:

"(d) kupendekeza kupandisha vyeo wafanyakazi wa Ofisi".

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**47.** Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Bodi, kumsimamisha au kufuta uteuzi wowote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ikiwa kufanya hivyo kutakuwa ni kwa maslahi ya umma".

Marekebisho ya kifungu cha 20.

**48.** Kifungu cha 20 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa aya ya (d) na kuwekwa aya mpya ya (d) kama ifuatavyo:

"(d) kuwasilisha ripoti kwa Mthibiti Ubora na kwa Mamlaka husika kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 8 cha Sheria hii".

Marekebisho ya kifungu cha 22.

**49.** Kifungu cha 22 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa aya ya (c) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (c) kama ifuatavyo:

"(c) kuandaa ripoti za skuli na ripoti za Mwalimu mmoja mmoja na kuziwasilisha kwa Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa".

Marekebisho ya kifungu cha 32.

**50.** Kifungu cha 32 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa vifungu vidogo vya (2) na (4).

Marekebisho ya Jadweli.

**51.** Jadweli la Sheria Mama linarekebishwa katika kipengele cha 11 kwa kufutwa vipengele vidogo vya (1) na (2) na kuwekwa badala yake vipengele vidogo vipya vya (1) na (2) kama ifuatavyo:

"(1) Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zake, kuanzisha kamati kufanya kazi mahsusi kama itakavyopewa na Bodi.

(2) Utaratibu, vigezo na mambo mengine yanayohusiana na kamati hizo zitakazoanzishwa utakuwa kama utakavyoelekezwa na Bodi".

# SEHEMU YA KUMI
# MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

Kusomwa.

**52.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**53.** Kifungu cha 26 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa:

(a) kufutwa maneno "mafao ya matibabu" katika aya ya (e) na kuweka badala yake maneno "fao la upotevu wa ajira";

(b) kuongezwa aya mpya ya (f) mara baada ya aya ya (g) kama ifuatavyo:

"(f) fao la kuumia kazini";

(c) kuwekwa upya nambari ya aya (f) kuwa aya (g).

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**54.** Kifungu cha 29 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa vifungu vidogo vya (4), (5) na (6) na kuwekwa badala yake kifungu kidogo kipya cha (4) kama ifuatavyo:

"(4) Mwanachama anastahili kulipwa fao la upotevu wa ajira kutoka katika Mfuko, iwapo:

(a) amechangia katika Mfuko kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na nane (18);

(b) ajira yake imefikia ukomo au amepoteza ajira kwa sababu yoyote ile isipokuwa kuacha kazi kwa hiari yake mwenyewe au kuachishwa kazi kwa sababu ya rushwa, ubadhirifu au kuacha kazi kwa kushiriki katika shughuli za kisiasa kwa mujibu wa Sheria ya Watumishi wa Umma (Kushiriki katika Shughuli za Kisiasa), Nam. 3 ya mwaka 2003;

(c) amepoteza ajira kwa kipindi kisichopungua miezi sita (6);

(d) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(e) atathibitisha kwa Mkurugenzi Mwendeshaji kwa kiapo kuwa hana ajira nyengine, kutoka Tume ya Utumishi na Kamisheni ya Kazi ya Zanzibar; na

(f) ana umri chini ya miaka hamsini na tano (55)".

(b) katika kifungu kidogo cha (9), kufutwa nambari ya rejea "(8)" na badala yake kuwekwa nambari mpya ya rejea "(6)";

(c) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (7) kuwa kifungu kidogo cha (5), kifungu kidogo cha (8) kuwa kifungu kidogo cha (6) na kifungu kidogo cha (9) kuwa kifungu kidogo cha (7).

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**55.** Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa kifungu kidogo cha (6) na kuwekwa badala yake kifungu kidogo kipya cha (6) kama ifuatavyo:

"(6) Iwapo mwanachama amefanya kazi kwa kipindi fulani na akapoteza ajira yake kutokana na mkataba wa ajira yake kumalizika au kuachishwa kazi, atastahiki kulipwa fao la upotevu wa ajira kwa mujibu wa Kanuni".

(b) kufutwa kifungu kidogo cha (7).

Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.

**56.** Jadweli la Kwanza la Sheria Mama linarekebishwa katika kipengele cha 2 kwa kufutwa aya ya (c) na kuwekwa aya mpya ya (c) kama ifuatvyo:

"(c) fao la upotevu wa ajira 2%".

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA VYOMBO VYA MOTO VYA SERIKALI, NAM. 13 YA MWAKA 2004

Kusomwa.

**57.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Vyombo vya Moto vya Serikali, Nam. 13 ya 2004 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**58.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufutwa ufafanuzi wa neno "Waziri Kiongozi".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**59.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufutwa maneno "na Waziri Kiongozi" na kuwekwa badala yake maneno "Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais".

Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.

**60.** Jadweli la Kwanza la Sheria Mama linarekebishwa katika kipengele cha 1(1) kwa kufutwa aya ya (c) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (c) kama ifuatavyo:

"(c) Msajili wa Hazina".

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUMO WA UDHIBITI WA LESENI ZA BIASHARA, NAM. 13 YA 2013

Kusomwa.

**61.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfumo wa Udhibiti wa Leseni za Biashara, Nam. 13 ya 2013 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**62.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa:

(a) kufutwa aya ya (a) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (a) kama ifuatavyo:

"(a) kuendeleza, kutekeleza na kuendesha Mfumo wa Kitaifa wa Leseni".

(b) kuongezwa aya mpya za (o) na (p) mara baada ya aya ya (n) kama ifuatavyo:

"(o) kudhibiti, kufuatilia na kusimamia Mamlaka za Leseni kutumia mfumo katika kutoa leseni, vibali na uthibitisho mwengine;

(p) kutoza ada za udhibiti kutoka Mamlaka za Leseni kwa ajili ya uendeshaji wa mfumo wa leseni".

Marekebisho ya kifungu cha 51.

**63.** Kifungu cha 51 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongezwa aya mpya ya (d) kama ifuatavyo:

"(d) makusanyo ya fedha zinazotokana na huduma zilizotolewa na Baraza katika kutekeleza kazi zake".

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA, NAM. 3 YA 2016

Kusomwa.

**64.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, Nam. 3 ya Mwaka 2016 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**65.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (5).

Kuongeza kifungu kipya cha 5A.

**66.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 5A mara baada ya kifungu cha 5 kama ifuatavyo:

Katibu wa Bodi.

**5A.-**(1) Bodi itamteua Afisa wa Umma ambaye atakuwa na sifa zifuatazo kuwa Katibu wa Bodi:

(a) awe ana angalau Shahada ya Kwanza katika Taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) awe muadilifu wa hali ya juu;

(c) awe na uwezo wa kutumia vifaa vya teknolojia na habari; na

(d) awe anaweza kutunza siri.

(2) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na:

(a) atachukuwa kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(b) atatunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(c) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa Wajumbe;

(d) atatoa ushauri sahihi kwa Bodi pale ambapo utahitajika; na

(e) atafanya kazi nyengine zozote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 22 Juni, 2022.

.........................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***